# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

(nembo)

**SHERIA NDOGO**
**(USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA ZA MWAKA 2017**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982**

***(SURA YA 290)***

**SHERIA NDOGO**

**YALIYOMO**

.

1. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Eneo la matumizi

3. Tafsiri

4. Utozaji ushuru

5. Utunzaji wa kumbukumbu

6. Uwasilishaji wa kumbukumbu

7. Taarifa ya kuwasilisha hesabu na kulipa ushuru

8. Uwezo wa kuingia kwenye jengo

9. Wajibu wa mlipaji

10. Uteuzi wa mkusanya ushuru

11. Tathmini ya hesabu

12. Riba kwa ushuru usiolipwa

13. Makosa

14. Adhabu

15. Kufifilisha kosa

**TANGAZO LA SERIKALI NA………LA TAREHE ………………………..**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982**

***(SURA YA 290)***

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6 (1) na 13 (1)*

## SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA ZA MWAKA 2017

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Maswa za mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. *Jina na mwanzo wa kutumika*

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. *Eneo la matumizi*

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo: *Tafsiri*

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri ya Jiji kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Maswa.

"Hesabu" maana yake jumla ya mauzo au matumizi ikiwa ni pamoja na ushuru na ada katika mwaka;

"Hesabu za mwisho" maana yake ni jumla ya mauzo na matumizi yanayowasilishwa na taasisi yoyote ya kibiashara au mtu binafsi baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa aya ya 9 ya Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Jumuisho' maana yake taarifa, nyaraka, hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizowasilishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa au kuuzwa kibiashara ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho.

"Kipindi cha hesabu" maana yake muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake.

“Mkurugenzi” maana yake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Mlipaji” maana yake ni taasisi / kampuni ya kibiashara au mtu yeyote anayefanya biashara mwenye leseni ya biashara na itajumuisha Tawi/Matawi ya Mlipaji linalofanya shughuli za Kiuchumi/Biashara ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.

“Mwaka wa mapato” maana yake kipindi cha miezi kumi na miwili ya kalenda ya mwaka.

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura 290 ya mwaka, 2002

“Taasisi ya Kibiashara” maana yake taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni au Sheria ya Usajili wa Majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma au biashara yoyote ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na inayofanya shughuli hizo ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Maswa.

“Ushuru wa huduma” maana yake ni tozo ya asilimia Sifuri nukta Tatu (0.3%) inayolipwa na Mlipaji kutokana na Hesabu za shughuli zote baada ya kuondoa Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya Mlaji.

“Wakala” maana yake ni mtu, taasisi au kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

4 (1) Halmashauri itatoza ushuru wa huduma kwenye taasisi au makampuni na mtu yeyote anayefanya biashara mwenye leseni ya biashara kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mapato ghafi baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji. *Utozaji ushuru*

Isipokuwa, matawi ya makampuni yatalipa ushuru wa huduma kwa mamlaka za wilaya / miji ambako matawi hayo yapo.

(2) Ushuru wa huduma kwa mujibu wa kifungu hiki utatozwa kwa makundi yafuatayo;-
(a) Kila taasisi au kampuni ya biashara,
(b) Tawi la taasisi au kampuni ya biashara ambalo lipo katika eneo la Halmashauri,
(c) Mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara.

5 (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mlipaji kutunza kumbukumbu za biashara yake; *Utunzaji wa kumbukumbu*

(2) Mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye atashindwa kuonesha kumbukumbu na hakuna namna ya kupata taarifa zake atalipa ushuru wa huduma kiasi cha shilingi elfu thelathini kwa mwaka.

6 (1) Halmashauri inaweza kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mlipaji wa ushuru wa huduma au wakala kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya ushuru wa huduma; *Uwasilishaji wa kumbukumbu*

(2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) Halmashauri inaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhiniwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

7 (1) Halmashauri inaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka Mlipaji wa ushuru kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli zilizowasilishwa, kutolewa, kuingizwa kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku kumi na nne tangu tarehe ya taarifa hiyo; *Taarifa ya kuwasilisha hesabu na kulipa ushuru*

(2) Halmashauri inaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa mlipaji kumtaka alipe ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

8 Mkurugenzi anaweza kumwagiza Afisa Muidhiniwa au Wakala kuingia kwenye jengo au eneo la taasisi ya kibiashara au la mlipaji au kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za kibiashara, vitabu vya hesabu na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha *Uwezo wa kuingia kwenye jengo*

ushuru wa huduma anachotakiwa kulipa mlipaji wa ushuru wa huduma au wakala.

9 (1) Kila mlipaji atatakiwa kutoa au kuwasilisha hesabu za mwisho za mwaka uliopita na kuziwasilisha bila adhabu kuanzia tarehe moja mwezi Januari hadi tarehe kumi na tano mwezi Januari kila mwaka. *Wajibu wa mlipaji*

(2) Kila mlipaji atatakiwa kulipa ushuru wa huduma bila adhabu kuanzia tarehe moja mwezi Januari hadi tarehe thelathini mwezi Machi kila mwaka.

(3) Itakuwa ni kosa kutowasilisha hesabu za mwaka na kutolipa ushuru wa huduma kwa wakati.

(4) Iwapo mtu yeyote atasema uongo au ataficha baadhi ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha ushuru wa huduma anachotakiwa kulipa, mtu huyo atatozwa ushuru wa huduma anaotakiwa kulipa pamoja na nyongeza ya ushuru ya asilimia hamsini ya tofauti kati ya kodi anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha.

(5) Endapo muda wa kuwasilisha taarifa na kulipa ushuru kwa mujibu wa kifungu hiki utapita bila malipo kufanyika Halmashauri itachukua hatua kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

10 Halmashauri inaweza kumteua Afisa Mwidhiniwa kutathmini na kukusanya ushuru wa Huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa na Sheria Ndogo hizi kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata ushuru pamoja na madeni yake; *Uteuzi wa mkusanya ushuru*

11 (1) Mlipaji anapowasilisha hesabu zake, Halmashauri inaweza; *Tathmini ya hesabu*

(a) Kupokea na kukubali hesabu hizo na kutathimini ushuru wa huduma katika msingi huo au;

(b) Kufanya tathmini na kuamua kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa ushuru wa huduma hiyo iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi;

(2) Endapo mlipaji hatawasilisha hesabu za mwisho katika mwaka husika, au ametasilisha taarifa yenye mashaka Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuomba taarifa kutoka kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

(3) Baada ya tathmini kukamilika mlipaji atapaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

12 (1) Ushuru ambao haujalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia moja nukta tano (1.5) kwa mwezi au shilingi elfu hamsini kwa mwezi kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa na itatakiwa kulipwa na mlipaji; *Riba kwa ushuru usiolipwa*

(2) Riba itakayotozwa katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama ushuru unaostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama ushuru unaolipwa na mlipaji.

13 Mtu yeyote au mlipaji yeyote:- *Makosa*

(a) Atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi kwa wakati;
(b) Atashindwa kulipa ushuru kwa wakati;
(c) Atashindwa kuwasilisha nyaraka, au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa na Sheria Ndogo hizi;
(d) Atashindwa kutunza na kuonesha kumbukumbu kwa Halmashauri kwa ajili ya uchunguzi.
(a) Atatoa hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi;
(b) Atatoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa ushuru;
(c) Atandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au

kumbukumbu;

(d) Atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa Muidhiniwa kutekelewa majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi

atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

14 (1) Mtu yeyote au mlipaji yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo. Adhabu

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika kifungu cha 20 (1) mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia katika kudai ushuru wa huduma, kutokana na kuvunja Sheria Ndogo hizi na kulipa deni analodaiwa.

15 Endapo mtu yeyote ametenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi atafifilisha kosa na kuagiza kuwa mtu / mlipaji huyo alipe deni analodaiwa pamoja na adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi Elfu Hamsini (Tsh.50,000/=). *Kufifilisha kosa*

JEDWALI LA KWANZA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA .................**

HATI NA. ………….. Tarehe………………….

**FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**

***(****Chini ya kifungu cha 15 cha Sheria ndogo hizi)*

Mimi ……………………….…....................…………………………….…..... nakiri mbele ya ……………………………………...........……. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kwamba mnamo tarehe ….…  ya Mwezi …...…. Mwaka …..........… nilitenda kosa la kukiuka maelekezo ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya ............................ (Ada na Ushuru) za Mwaka 2011; sasa nipo tayari kulipa faini kiasi cha Sh…………………………………… ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni ya kweli nimeyatoa kadri ya ufahamu wangu leo tarehe………………………….Saini………………………………………….

**AFISA MUIDHINIWA**
Nimepokea kiasi cha Sh……………………………… toka kwa mtajwa hapo juu na nimemkatia risiti namba………………………………………………..
Jina: ……………………………………………
Cheo: ………………………………………….
Saini: …………………………………………..

Lakiri ya Halmashauri ya ............................ imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya .................... kilichofanyika tarehe ................ Mwezi .........., mwaka ......... na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikibandikwa mbele ya:

……. …………………………………..
(JINA)
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ...............

…..…………………………
(JINA)
MWENYEKITI WA HALMASHAURI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ..............

NAKUBALI,

………………………………………...

GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)
WAZIRI WA NCHI –OR-TAMISEMI

**DODOMA**

*TAREHE: ………………………..*